**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# SHULE YA SEKONDARI MWISI

**S.L.P 173, IGUNGA. SIMU +255767066073/693469292**

Kwa mzazi/mlezi wa: ............................................................

S.L.P.................................................................

...................................................................

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWISI KIDATO CHA TANO (V) MWAKA 2022/2023**

**UTANGULIZI.**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari **MWISI** kidato cha Tano mwaka **2022/2023** kwa chaguo la………… (**tahasusi)** Shule itafunguliwa tarehe …………………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………. Tarehe ya kufungua/kuripoti shuleni inaweza kubadilika kutegemea na maagizo ya waziri mwenye dhamana.

**1 KUFIKA ILIPO SHULE:**

Shule ipo umbali wa kilometa **83** kutoka **Igunga Mjini** na kilometa **45** kutoka **nzega mjini**. Usafiri wa daladala/basi kuja **Mwisi** kutoka **Igunga Mjini** unapatika **stendi ya Mabasi Igunga** kwa shilingi **5000/=,**Ukitokea **Nzega Mjini** Kuja Mwisi usafiri wa daladala/basi unapatikana stendi **Mpya ya mabasi Nzega** kwa shilingi **4000/=** Pia unaweza ukashukia kituo cha **Ziba** ambacho kipo barabara kuu katikati ya Nzega na Igunga ambapo nauli ya kufika **Mwisi ni 3000/=.**Kutoka Tabora mjini kuja Mwisi nauli ni **Tsh 8,000/=**

**2 ADA NA MICHANGO YA SHULE**

Ada na baadhi ya michango inatakiwa ilipwe kupitia akaunti ya NMB ya shule yenye jina la **MWISI SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT – 50901100042**.Mwanafunzi lazima alete fomu aliyotumia kuwekea fedha benki (Bank Pay In Slip-BPS) inayoonesha umelipia Ada/michango hiyo.Hakikisha majina kamili ya mwanafunzi na kidato vinaonekana kwenye Bank Pay In Slip.

**NB;**Shule haipokei fedha Taslimu,fedha zote zilipwe kupitia benki ya NMB tawi lolote kwa kutumia namba za akaunti iliyotajwa hapo juu.

**JEDWALI LA UFAFANUZI WA ULIPAJI WA KARO NA MICHANGO MINGINE YA SHULE**

| S/N | FEDHA KWA AJILI YA | KIASI KWA MWAKA | KIASI KWA MHULA |
|---|---|---|---|
| 01 | Ada | 70,000/= | 35,000/= Benki |
| 02 | Taaluma | 20,000/= | 10,000/= Benki |
| 03 | Tahadhari(haitarudishwa) | 5,000/= | Lipa yote benki |
| 04 | Mchango wa wapishi/walinzi/vibarua | 30,000/= | Lipa yote benki |
| 05 | Ukarabati wa Samani | 25,000/= | Lipa yote benki |
| 06 | Kitambulisho na picha | 6,000/= | Lipa yote benki |
| 07 | CHF na Huduma ya kwanza | 10,000/= | Lipa yote benki |
| 08 | Nembo | 2,000/= | Lipa yote benki |
| 09 | Mitihani ya kujipima(Mock) | 20,000/= | Lipa yote benki |
| 11 | Fagio la nje la chelewa (1) | Alete | |
| 12 | Soft broom (1) | Alete | |
| 13 | Hard broom(1) | Alete | |
| 14 | Mopper(1) | Alete | |
| 15 | Jembe na mpini wake (1) | Alete | |
| 16 | Fyekeo (1) | Alete | |
| 17 | Ndoo kubwa (1) | Alete | |
| 19 | Folder file kwa ajili ya taarifa zake(1) | Alete | |
| 20 | Picha(2) za passport size za mzazi | Alete | |

**NB;** Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vya kutosheleza vya kujifunzia madarasani;yaani madaftari makubwa(Counter Books Quire 3) ya kutosha masomo atakayosoma pamoja na vifaa vingine kama kikokotoo(scientific calculator),Dissecting Kit,Pakti moja ya Gloves, "Laboratory coat," 'stop watch'na 'thermometer' na begi moja jeusi la kubebea madaftari yake.

Ili kuepusha usumbufu wa kubeba vifaa vingi wakati unasafiri kuja shule tunashauri uje ununue vifaa katika maduka yanayopatikana Mwisi,vifaa vinavyopatikana katika maduka ya Mwisi ni madaftari makubwa,scientific calculator,File,fagio la nje,Soft broom,Hard broom,Ndoo kubwa,jembe na mpini.

## 3 SARE ZA SHULE

### 3.1 WASICHANA

1. Sketi 2 za ***Dark Blue*** kitambaa kizito cha suti marinda 14 ya kupanga iwe ndefu hadi katikati ya goti na jicho la mguu(ankle) na mkanda wake usizidi inchi 2 na isiwe ya kubana.
2. Shati 2 nyeupe za tetron mikono mifupi zisizobana
3. Tai ndefu ya Dark Blue
4. Kwa waislamu Sketi ndefu zifike kwenye jicho la mguu,nusu kanzu nyeupe pamoja na juba jeupe linaloishia tumboni
5. Soksi nyeupe za stockings jozi 2 zisizoonesha mwili
6. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba pea 2,viwe vya kupigwa kiwi na visivyo na kisigino kirefu na urembo wowote.
7. Sweta 2 za Blue zenye V-shape

### 3.2 WAVULANA

1. Suruali 2 za ***Dark Blue*** kitambaa kizito cha suti ,isiwe ya kubana yenye marinda 2 kushoto na marinda 2 kulia,iwe na mifuko 2 mbele na 1 nyuma.iwe na turn up chini na isiwe modo.
2. Shati 2 nyeupe za tetron mikono mifupi zisizobana
3. Tai ndefu ya Dark Blue
4. Soksi nyeupe jozi 2
5. Vest/singlet 2 nyeupe za kuvalia ndani ya shati
6. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba pea 2,viwe vya kupigwa kiwi na visivyo na visigino virefu na urembo wowote.
7. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
8. Sweta 2 za Blue zenye V-shape

### 3.3 VIFAA VYA MICHEZO KWA WOTE

1. Tracksuit ya rangi ya Bluu yenye mistari myeupe ubavuni (Rangi ya Chelsea F.C)
2. Tshirt ya michezo ya rangi ya Bluu jozi 2 (Rangi ya Chelsea F.C)
3. Bukta ya rangi ya Bluu
4. Raba nyeupe jozi 2

### 3.4 SARE YA JIONI

#### 3.4.1 WASICHANA

1. Sketi 2 za ***Maroon(Damu ya mzee iliyokolea)*** kitambaa kizito cha suti marinda 14 ya kupanga iwe ndefu hadi katikati ya goti na jicho la mguu(ankle) na mkanda wake usizidi inchi 2 na isiwe ya kubana.

#### 3.4.2 WAVULANA

1. Suruali 2 za ***Maroon(Damu ya mzee iliyokolea)*** kitambaa kizito cha suti ,isiwe ya kubana yenye marinda 2 kushoto na marinda 2 kulia,iwe na mifuko 2 mbele na 1 nyuma,iwe na turn up chini na isiwe modo.

## 4 MAHITAJI YA BWENINI

Vifaa vifuatavyo ni vya lazima mwanafunzi kuja navyo shuleni kwa ajili ya matumizi ya bwenini

a) Godoro moja inchi $2\frac{1}{2}$ x 6
b) Shuka 2 za **light blue** na 2 za **pink**
c) Blanket 1 kwa ajili ya baridi
d) Chandarua cha bluu pamoja na mto (rangi za foronya za mito zifanane na rangi za mashuka)
e) Tranker moja la kuwekea vifaa vyake bwenini
f) Ndoo ndogo 2 za plastic(10 ltrs)
g) Dumu la maji ya kunywa ( 5 ltrs)
h) Vyombo vya chakula: Sahani yenye vyumba vyumba ya chuma ( Aluminium Tray),Kikombe na Kijiko
i) Tochi ndogo ya betri au Solar
j) Aje na toilet paper 10 kwa ajili ya matumizi yake zitakaguliwa siku anaripoti

**NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mizigo mingi Zaidi ya begi moja dogo la mgongoni na sanduku moja la chuma(Tranka) kwani hakuna sehemu ya kuhifadhi mizigo mikubwa.**

## 5 ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI ( COMBINATION )

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na vitabu vifuatavyo atakavyovitumia katika masomo yake,ni muhimu sana kuzingatia hili

### 5.1 CHEMISTRY REFERENCE BOOKS

1. Jain. S.K, (2010), *Conceptual chemistry For Class x1*, S. Chand & Company Ltd, New Delhi, India.
2. Mkayula, L.L et al (1998), *Phyisical Chemistry, Volume 1*, (Mzumbe Book Project), Mzumbe, Tanzania.
3. Bahl. B.S et al (2009), *Essentials of Physical Chemistry*, S. Chand & Company Ltd, New Delhi, India.
4. Ramsden. E.N, (2000), *A – Level Chemistry, 4$^{th}$ Ed*, Nelson Thornes Ltd, U.K.

### 5.2 BIOLOGY REFERENCE BOOK.

1.Taylor D.J, (1999), *Biological Science*, 3$^{rd}$ Ed, Cambridge University Press London.

### 5.3 GEOGRAPHY BOOKS

1. Mcknight, T, (2008), Physical Geography A L and scape appreciation, prentice Hall USA.
2. Pritchard, J, (1984), *Practical Geography For Africa*, Longman group U.K.
3. Bunnet, R. (1973), *General Geography in Diagram*, Education Singapore.
4. Monkhouse, F (1975), *Principale of Physical Geography*, Education Hodder, UK.

## 6 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995.Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

### 6.1 UNATAKIWA KUZINGATIA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO;

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa amkini kufanya maandalio jioni(preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli ya shiule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Hauruhusiwi kunyoa kipara,kufuga nywele ndefu,kufuga kucha ndefu,kupaka midomo na kucha rangi,kutinda nyusi,kupaka wanja,kuvaa herein,bangili,mikufu,nguo fupi na nguo zisizo na heshima na adabu.
i) Fanya kila kazi halali kwa maendeleo ya Shule na Taifa.Asiyejiweza kwa sababu ya maradhi;mzazi au mlezi atume taarifa ya daktari inayothibitisha Afya kwa Mkuu wa Shule.
j) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.

### 6.2 SEHEMU AMBAZO WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFIKA BILA KIBALI

- Chumba cha walimu (Staff room)
- Maabara
- Ofisi ya shule
- Jikoni
- Nyumba za walimu na wafanyakazi

### 6.3 SEHEMU ZILIZOPIGWA MARUFUKU WANAFUNZI KUTEMBELEA.

- Vilabu vya pombe.
- Majumba ya starehe (Clubs)
- Nyumba za kulala wageni.
- Sehemu za michezo ya pool table na Kamari

## 6.4 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati,Ubakaji,Ushoga na Usagaji
c) Kutokuhudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi,kubeli n.k
e) Kupigana au Kupiga
f) Kuharibu makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito au kusababisha mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzanko,walimu,walezi na jamii kwa ujumla,
l) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
m) Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule
n) Kukataa adhabu kwa makusudi
o) Kuwa na simu ya mkononi

## 7 MAMBO MENGINE MUHIMU

Mwanafunzi anaporipoti anatakiwa aje na Mzazi/Mlezi pamoja na fomu hizi za maagizo ya kujiunga na shule zikiwa zimejazwa vinginevyo hatopokelewa.Fomu zote zijazwe kama ilivyo elekezwa na anatakiwa kuzikabidhi kwa makamu Mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.

a) **Fomu Na. 1: Ahadi ya mzazi/mlezi:** Fomu hii itajazwa na Mzazi/Mlezi.
b) **Fomu Na. 2: Kiapo cha Mwanafunzi:** Fomu hii itajazwa na Mwanafunzi.
c) **Fomu Na. 3:Kiapo cha Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**Fomu hii itajazwa na Mzazi/Mlezi.
d) **Fomu Na. 4: Medical Examination Form**Fomu hii itajazwa na Daktari wa hospitali ya serikali.

NB: Shule haitoi chakula maalumu **(special diet),**hivyo chakula kitakachopikwa jikoni ndicho kitakacholiwa na wanafunzi wote.Hairuhusiwi kula chakula nje ya shule hii ni kwa usalama wa Afya ya Mwanafunzi.Soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na uyatekeleze kikamilifu.

**KUMBUKA**

**Simu haziruhusiwi kabisa shuleni,mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.Mwanafunzi awapo safarini atumie simu ya dereva.Kwa mawasiliano piga simu 0782 854 293 (Makamu Mkuu wa shule)**

**KARIBU SANA MWISI SEKONDARI**

…………………………………….

**ABDULLAH M.MUNKUNDA**
**MKUU WA SHULE**

FOMU NA. 1. **AHADI YA MZAZI / MLEZI**

Mimi.........................................................S.L.P.................Mji........................Simu.............
...........Ambaye kazi yangu ni ................................. natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ................................................Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya Sekondari MWISI kuanzia tarehe ...........................Nina ahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa maswala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina....................................................................saini...............tarehe...................................

Uhusiano na mwanafunzi................................

**FOMU NA.2**

## KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ……………………………………………….Wa kidato cha Tano chaguo la ……………… (tahasusi) mwaka 2020 / 2021.Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari MWISI. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na taifa langu.Naapa kuwa sitoshiriki wala kuanzisha Mgomo wa aina yoyote kwa muda wote nitakao kuwepo shuleni.Endapo nikishiriki au kuanzisha Mgomo wa aina yoyote naomba sheria kali ichukuliwe dhidi yangu.

Ee Mola nisaidie.

Jina…………………………………….....saini…………………..Tarehe……………..

**Maoni ya Mkuu wa Shule**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**FOMU NA. 3**

**KIAPO CHA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………mzazi/mlezi wa…………………………………wa S.L.P………………Mji……………………… Simu…………………Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu wanne(4) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

1. Jina…………………………Simu………………uhusiano…………………

2. Jina ………………………… … Simu………………. uhusiano………………

3. Jina……………………………… Simu……………… uhusiano………………

4. Jina………………………………Simu………………uhusiano………………

***SAINI YA MZAZI/MLEZI…………………………Simu………………………***

**FOMU NA. 4**

MWISI Secondary School,

P.O. BOX 173, IGUNGA.

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name ……………………..……………Age………..Sex………year………………..

Height …………….. Weight…………..

1. Blood count (Red and White) ………………………………………….. ………..
2. Urine analysis Test ……………………………………………………………………..
3. Syphilis test ………………………………………………………………………………….
4. T.B. ……………………………………………………………………………………………
5. Eye Test ………………………………………………………………………………………..
6. Ears ……………………………………………………………………………………………
7. Spleen ………………………………………………………………….. ………………
8. Abdomen………………………………………………………………….. ……………….
9. Cardiovascular system: Blood pressure: systolic: …………………………

Heart: Any murmur……………………………………

Arteries and Veins……………………………………

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is / not fit to pursue studies at MWISI Secondary school.

……………………………………..  ………………………………………

Name and Designation  Signature and Official stamp

…. ……...…………………………  ………………………

STATION  DATE

NOTE:

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.